

### Tanzia

Hizb ut-Tahrir / Wilayah Uturuki Yamuomboleza Vedat Kurnaz,  
Mmoja wa Mashababu Wake Wenye Ikhlas!  
(Imetafsiriwa)

﴿مِنَ الْمُؤْمِنِينَ رِجَالٌ صَدَقُوا مَا عَاهَدُوا اللَّهَ عَلَيْهِ فَمِنْهُمْ مَّن قَضَىٰ نَحْبَهُ  
وَمِنْهُمْ مَّن يَنْتَظِرُ وَمَا بَدَّلُوا تَبْدِيلًا﴾

"Miongoni mwa Waumini wapo watu walio timiza waliyo ahidiana na Mwenyezi Mungu. Baadhi yao wamekwisha kufa, na baadhi wanangojea, wala hawakubadilisha (ahadi) hata kidogo." [Ahzab: 23]

Vedat Kurnaz alijitolea maisha yake kama Muislamu mwenye ikhlasi na mwaminifu aliyefanya kazi ya kuregesha tena maisha kamili ya Kiislamu, kisha akamaliza maisha yake ambayo aliyatumia kubeba ulinganizi wa Kiislamu na yeye pia akiwa ni mbebaji ulinganizi huu, ambapo alikufa katika masaa ya jioni kutokana na shambulizi la moyo (angina pectoris) alipokuwa akitoa halqa (duara la masomo) kwa Mashababu.

Marehemu Vedat Kurnaz alizaliwa mnamo 1966, yeye ni mhandisi wa umeme na vifaa vya kielektroniki, na alikuwa ni mjumbe wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut-Tahrir katika Wilayah ya Uturuki. Alianza kufanya kazi ya da'wah huko Vienna na kisha Uturuki. Alitumia maisha yake katika da'wah ya kurudisha tena maisha kamili ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume. Na vile vile aliondoka kwenda katika rehema ya Mwenyezi Mungu (swt) ilhali anatoa halqa ya masomo ya kusimamisha hukmu ya Mwenyezi Mungu katika ardhi, na sisi tunashuhudia hilo mbele ya Mwenyezi Mungu (swt).

Tunamwomba Mwenyezi Mungu (swt) amminie ndugu yetu mpendwa rehema yake na aipe ilham familia yake kwa subra njema, na tunatanguliza rambi rambi zetu kwa jamaa zake, wapendwa wake na wenzake walio katika njiani kwake.

﴿إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ﴾

"Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake Yeye hakika tutarejea." [Baqara: 156]

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir  
katika Wilayah Uturuki